

## TANZU ZA FASIHI SIMULIZI

M.M. Mulokozi

### Utangulizi

Ingawa fasihi simulizi tumekuwa nayo kwa maelfu ya miaka, lakini imeanza kuchunguzwa kisayansi na kufundishwa mashuleni siku za karibuni tu. Kwa sababu hii, taaluma yake bado ni changa; hatujawa na marejeo, nadharia wala istilahi zenye kutosheleza mahitaji ya taaluma hii.

Tatizo hili linadhihirika mara moja tunapoangalia kazi za wataalamu mbali mbali kuhusu "tanzu za fasihi simulizi." Kwa upande wa nadharia, kitabu pekee kinachozijadili kwa urefu tanzu za fasihi simulizi za Afrika ni kile cha Ruth Finnegan *Oral Literature in Africa* (1970). Upande wa Kiswahili, hatuna kitabu hata kimoja kinachoujadili uwanja huu kwa undani. Badala yake tunayo miongozo michache kwa ajili ya shule za sekondari (Balisidya, N. 1975; Kirumbi, 1977; Taasisi ya Elimu, 1976); yapo pia makala kadha wa kadha juu ya fasihi simulizi yaliyochapishwa katika vitabu na majarida, na tasnifu, kwa mfano Mbele (1980), Balisidya (Matteru) 1979; 1983), Kamera (1983), Mulokozi (1983, 1983a, 1987), TUKI (1977, 1982), Msuya (1979) TAKILUKI (1983) na Mlacha (1985).

Makala yote haya yametoa mchango fulani katika kueneza taaluma ya fasihi simulizi katika Tanzania, lakini bado tunahitaji maandishi mengi zaidi yanayotokana na utafiti wa uwandani.

Ingawa machapisho yanazidi kuongezeka, lakini bado hazijajitokeza kazi zenye kutusogeza mbele kitaaluma kuvuka pale walipotufikisha Finnegan (1970) na Balisidya (Matteru) (1975; 1987). Maandishi hayo ni majaribio ya mwanzo ya kuainisha (*classify*) na kuelezea tanzu za fasihi simulizi, hatua ambayo ni ya lazima katika kuifanya taaluma ya fasihi simulizi iwe sayansi.

Mambo muhimu yanayojitokeza katika makala ya Finnegan na Balisidya ni kwamba:

- a) Afrika ina utajiri mkubwa wa fasihi simulizi iliyojevuka;
- b) Idadi ya tanzu za fasihi simulizi ni kubwa na hubadilika kati ya jamii na jamii.
- c) Tanzu za fasihi simulizi huingiliana;
- d) Fasihi simulizi hubadilika badilika (hunyumbuka) kutegemea muktadha wa utendaji

Ni muhimu kuyakumbuka mambo haya wakati tunapojadili tanzu za fasihi simulizi.

Makala haya ni jaribio la kuzigawa fani za fasihi simulizi ya Tanzania katika tanzu zake mahsusi kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

1. Umbile na tabia ya kazi inayuhusika
2. Muktadha na namna ya uwasilishwaji wake kwa hadhira (hili linazingatia pia dhima yake ya kijamii);

Kwa upande wa umbile na tabia ya kazi ya sanaa tunaangalia vipengele vya ndani vinavyoiumba sanaa hiyo na kuipa mwelekeo au mwenendo ilio nao. Baadhi ya vipengele hivyo ni namna lugha inavyotumika (kishairi, kinathari, kimafumbo, ki-wimbo, kighani, n.k.), muundo wa fani hiyo, wahusika (kama wapo), n.k.

Kwa upande wa muktadha na namna ya uwasilishaji, tunazingatia ukweli wa msingi kuwa fasihi simulizi ni sanaa inayopita, isiyofungiwa katika umbo maalumu, wala matini maalumu, yasiyobadilika. Hivyo fasihi simulizi si kitu (*object*) bali ni tukio (*event*). Na kama matukio yote, inatawaliwa na mwingiliano wa vitu vitatu: Watu, wakati (*time*) na mahali (*space*). Mwingiliano huu ndio unaotupa muktadha, na muktadha ndio unaoamua fani fulani ya fasihi simulizi ichukue umbo lipi - iwasilishwe vipi kwa hadhira - kwenye wakati na mahali hapo. Hivyo hadithi inaweza kugeuzwa wimbo, utendi

unaweza kuwa hadithi, na wimbo unaweza kugeuzwa ghani au usemi kutegemea muktadha unaohusika. Jambo jingine la kukumbuka ni kwamba fasihi simulizi haikutengana na maisha bali ni sehemu ya maisha ya kila siku ya jamii zetu. Ingawa ni kweli kuwa zipo fani fulani chache ambazo zimekwisha jitenga na shughuli za maisha ya kila siku na kuwa ni matukio yanayojisimamia yenyewe, k.m. baadhi ya maghani kama vile tendi, lakini zilizo nyingi bado ni sehemu ya maisha. Fasihi za aina hiyo hukoleza matukio halisi ya kimaisha badala ya kuwa ni burudani tu ya kwenda kufurahia baada ya kazi. Kwa mfano, wazee wanapobarizi juu ya mambo muhimu ya kimaisha huweza kutumia fasihi simulizi katika umbo la methali, vitendawili, hadithi, nyimbo, na kadhalika. Wakulima wanapokuwa makondeni hutumia nyimbo kuchapusha kazi yao. Hii ni sababu mojawapo inayoleta ugumu katika kuzigawa fani za fasihi simulizi kitanzu.

Hata hivyo, pamoja na ugumu huu tulioutaja, katika makala haya tumejaribu kuzipanga fani za fasihi simulizi katika makundi mahsusi kwa mujibu wa vigezo tulivyovitaja hapo juu. Makundi hayo ni:

1. Mazungumzo
2. Masimulizi
3. Maigizo (Drama)
4. Ushairi a) Nyimbo  
b) Maghani
5. Semi
6. Ngomezi (tungo za ngoma)

*Tanzu na fani za fasihi simulizi*

#### 1. **MAZUNGUMZO**

Mazungumzo ni maongezi au maelezo ya mdomo, katika lugha ya kawaida, juu ya jambo lolote lile. Si kila mazungumzo ni fasihi. Ili mazungumzo yaitwe fasihi, lazima yawe na usanii wa aina fulani, yaumithilishe uhalisi badala ya kuunakili. Hali hii hujidhihirisha katika lugha, katika muundo na mtiririko wa mazungumzo yenyewe, na katika namna yanavyotolewa. Kwa mfano,

maongezi ya wazee katika baraza, hotuba zinazotolewa katika mazingira rasmi ya kimila (k.m. wakati wa kuposa), malumbano ya watani, ulumbi (*rhetoric*), na kadhalika ni mifano ya baadhi ya maongezi ambayo ni ya kifasihi.

Idadi ya tanzu zinazoingia katika fungu hili la mazungumzo ni kubwa, na hutofautiana kati ya jamii na jamii. Hapa tunaweza kutaja chache tu.

- a) Hotuba
- b) Malumbano ya watani
- c) Ulumbi (usemaji wa ufasaha na madoido)
- d) Soga
- e) Mawaidha

Vipengele hivi havihitaji maelezo mengi, kwani vinafahamika kwa wengi wetu. Labda la kuongeza hapa ni kwamba baadhi ya tanzu hizi za kimazungumzo huweza kuwa na fani kadha ndani yake. Kwa mfano malumbano ya watani ni dhana pana inayozingatia fani zifuatazo:

- (i) Utani wa mababu/mabibi na wajukuu
- (ii) Utani wa mashemeji
- (iii) Utani wa kikabila
- (iv) Utani wa marafiki, na kadhalika.

Kila mojawapo kati ya fani hizi huwa na kanuni zake, miktadha yake na mipaka yake katika jamii zinazohusika.

## 2. MASIMULIZI

Masimulizi ni fasihi yenye kusimulia habari fulani (*narrate*). Hivyo hii ni fasihi ya ki-hadithi na fani zake huwa na sifa zifuatazo:

1. Hueleza matukio katika mpangilio fulani mahsusi.
2. Huwa na wahusika, yaani watendaji au watendwaji, katika matukio yanayosimuliwa.
3. Hutumia lugha ya kimaelezo.
4. Utambaji au utoaji wake huweza kuambatana na

- vitendo au ishara.
5. Huwa na maudhui ya kweli au ya kubuni, na yenye funzo fulani kwa jamii.

Tanzu za masimulizi ni nyingi. Zinazofahamika zaidi hapa kwetu ni hizi zifuatazo:-

## **2.1 Tanzu za kihadithi (za kubuni)**

### **2.1.1 Ngano (vigano, hurafa)**

Hizi ni hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika kama wanyama, miti na watu kuelezea au kuonya kuhusu maisha. Utanzu huu unajumuisha fani kadha, kwa mfano:

- a) Istiara (*allegory*)  
Hadithi ambayo maana yake ya wazi inawakilisha maana nyingine iliyofichika (yaani hadithi nzima ni kama sitiari).
- b) Mbazi (*parable*)  
Hadithi fupi yenye mafunzo itolewayo kama kielelezo wakati wa maongezi au wa kumkanya mtu.
- c) Kisa (*Anecdote*)  
Hadithi fupi ya kufurahisha kuhusu tukio la kweli.

## **2.2 Tanzu za kisalua (kihistoria)**

### **2.2.1 Visakale (legends)**

Masimulizi ya mapokeo juu ya wahenga au mashujaa wa kabila au taifa yenye kuchanganya chuku na historia (k.m. hadithi ya Liyongo).

### **2.2.2 Mapisi**

Maelezo ya historia bila kutia mambo ya kubuni.

### 2.2.3 Tarihi (Chronicle)

Maelezo au jedwali ya matukio muhimu na tarehe zake. (Hii zaidi hutokea katika maandishi).

### 2.2.4 Kumbukumbu

Maelezo ya matukio muhimu yanayomhusu mtu binafsi au jamii ya watu. Fani za wasifu na tawasifu ni aina ya kumbukumbu. (Mifano ya kumbukumbu simulizi ambazo baadaye zimeandikwa katika vitabu ni J.Mbotela *Uhuru wa Watumwa*, Mzee Vincent D.Njovu, *Dereva wa Kwanza Tanganyika* (TPH) na Malcolm X *Autobiography* (Mh. A. Haley).

### 2.2.5 Visasili (Myths)

Tanzu zinazofungamana na imani za dini na mizungu (*rituals*) ya jamii. Visasili ni hadithi za kale zenye kuwakilisha imani na mtazamo wa jamii inayohusika kuhusu asili ya ulimwengu na mwenendo wake, kuhusu asili yao wenyewe, na maana na shabaha ya maisha yao. Mara nyingi hadithi hizi huaminiwa kuwa ni kweli tupu, na hutumika kuelezea au kuhalalisha baadhi ya mila na madhehebu ya jamii inayohusika.

## 3. MAIGIZO (DRAMA)

Drama, yaani maigizo yanayotumia watendaji kuiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine ili kuburudisha na kutoa ujumbe fulani, ni sanaa inayopatikana katika makabila mengi. Mara nyingi drama za Kiafrika huambatana na ngoma, utambaji hadithi au matendo ya kimila, kwa mfano jando na unyago. Yapo pia maigizo yanayofungamana na michezo ya watoto, matanga, uwindaji, kilimo na kadhalika. Drama nyingi hutumia maleba maalumu, k.m. vizuizui (*masks*).

Kwa ujumla, fani za maigizo bado hazija-shughulikiwa kwa undani katika taaluma ya fasihi simulizi. Zipo kazi chache tu zinazoujadili uwanja huu,

kwa mfano Hussein (1975) na Muhando na Balisidya (1976). Hivyo hili ni eneo ambalo linahitaji kufanyiwa kazi zaidi.

#### 4. Ushairi

Ushairi, katika fasihi simulizi, hupambanuliwa na lugha ya kawaida kwa namna unavyopanga na kutumia lugha na mbinu za kimuktadha. Kauli za kishairi hupangwa kwa kufuata wizani (*rhythm*) maalumu wa mawimbi ya sauti, na mara nyingi lugha ya mkato na mafumbo hutumika. Vile vile uimbaji au ughani (badala ya usemaji) pengine hutumika kuliwasilisha shairi kwa hadhira. Baadhi ya fani za ushairi huambatana na muziki wa ala, na wakati mwingine hupata wizani wake kutokana na mapigo ya muziki huo wa ala. Maana, hisia na hali ya kishairi hutokana na mwingiliano huu wa maneno (matini) na mazingira ya utendaji.

Kundi la ushairi lina tanzu nyingi, lakini tunaweza kuzigawa zote katika mafungu mawili: nyimbo na maghani.

##### 4.1 Nyimbo

Wimbo ni kila kinachoimbwa. Hivyo hii ni dhana pana inayojumlisha tanzu nyingi. Hata baadhi ya tanzu za kinathari, kama vile hadithi, huweza kuingia katika kundi la nyimbo pindi zinapoimbwa.

Mambo muhimu yanayotambulisha nyimbo ni:

- a) Muziki wa sauti ya mwimbaji au waimbaji;
- b) Muziki wa ala (kama ipo);
- c) Matini au maneno yanayoimbwa;
- d) Hadhira inayoimbiwa
- e) Muktdha unaofungamana na wimbo huo, kwa mfano sherehe, ibada, kilio n.k.

Baadhi ya tanzu za nyimbo zinazojulikana sana hapa Tanzania ni hizi zifuatazo:

#### 4.1.1. Tumbuizo

Hizi ni nyimbo za furaha ziimbwazo kuwafurahisha watu kwenye matukio mbalimbali, k.m. ngomani au harusini.

#### 4.1.2 Bembea (pembejezi)

Nyimbo za kubembeleza watoto. Mifano ni mingi, kila kabila wanazo.

#### 4.1.3 Kongozi

Nyimbo za kuaga mwaka (Waswahili)

#### 4.1.4 Nyimbo za dini

Kwa mfano kasida (za kumsifu mtume), nyimbo za wakristo, za ibada za jadi n.k.

#### 4.1.5 Wawe

Nyimbo za kilimo.

#### 4.1.6 Tenzi

Nyimbo ndefu za kimasimulizi au za mawaidha

#### 4.1.7 Tendi

Nyimbo ndefu za masimulizi juu ya matendo ya mashujaa.

#### 4.1.8 Mbolezi

Nyimbo za kilio au maombolezo.

#### 4.1.9 Kimai

Nyimbo zihusuzo shughuli za baharini (ki-maji).



#### **4.1.10 Nyiso**

Nyimbo za jandoni.

#### **4.1.11 Nyimbo za vita**

Nyimbo ziimbwazo na askari wakati wa vita.

#### **4.1.12 Nyimbo za uwindaji**

Huimbwa na makundi ya wawindaji na wasasi wakati wa shughuli au sherehe zao.

#### **4.1.13 Nyimbo za Taifa (anthems)**

Nyimbo za kusifia taifa au kabila.

#### **4.1.14 Nyimbo za watoto**

Nyimbo waimbazo watoto wakati wa michezo yao.

#### **4.1.15 Nyimbo za kazi**

Hili ni kundi kubwa la nyimbo. Karibu kila kazi ifanywayo na watu huwa na nyimbo zake k.m. kulima (taz. wawe), kutwanga, kupepetata, kusuka, kuchuuza, useremala, uvuvi, uashi, ufuaji chuma, uhunzi, na kadhalika.

#### **4.2 MAGHANI**

Maghani ni ushairi unaotolewa kwa kalima badala ya kuimbwa. Zipo aina mbili za maghani:

- (a) Maghani ya kawaida
- (b) Maghani ya masimulizi (*narrative*)

##### **4.2.1 Maghani ya kawaida**

Katika kundi hili tunaweza kuingiza fani mbalimbali za ushairi simulizi, kwa mfano ushairi wa mapenzi, siasa, maombolezo, kazi, dini, n.k. alimradi

ushairi huo unaghanwa badala ya kuimbwa au kusemwa tu.

#### 4.2.2 Sifo

Hili ni kundi mahsusi la maghani ambalo baadhi ya wataalamu wanafikiri ndilo lenye tungo zilizopevuka zaidi katika ushairi wa Waafrika (Finnegan, 1970:III).

Sifo ni tungo za kusifu. Nyingi husifu watu, lakini zipo nyingine zenye kusifu wanyama, mimea, au hata vitu tu. Baadhi ya sifo huwa zinakashifu au kukejeli vilevile. Baadhi ya tanzu muhimu za sifo ni: 1. Vivugo 2. Pembezi 3. Tondozi

##### 4.2.2.1 Vivugo (majigambo)

Kivugo ni ghani la kujisifia. Kwa kawaida hutungwa na kughanwa na mhusika mwenyewe. Kivugo hutungwa kwa ufundi mkubwa, kwa kutumia mbinu kama sitiari, vidokezi (*allusions*), ishara, takriri, na wakati mwingine hata vina.

Mjigambaji ambaye kwa kawaida ni mwanamume hujitungia shairi lake kufuatia au kufungamana na tukio maalumu katika maisha yake, kwa mfano kuingia jandoni, kuoja, kurejea kutoka vitani, kushinda jambo gumu, k.m. mnyama mkali, mchezo, kesi mahakamani, masomo, n.k.

Baadhi ya majigambo huwa ni marefu sana yenye masimulizi ndani, lakini mengi ni mafupi. Vivugo vingi hueleweka kwa urahisi kwa hadhira iliyokusudiwa, kwa vile huzungumzia mambo wanayoyafahamu au waliyoyashuhudia. Wale wasiohusika hupata taabu kuvielewa, hasa kama hawaifahamu vizuri historia ya mtunzi.<sup>2</sup>

Muundo wa kivugo hutegemea shabaha za mtunzi na jadi ya utunzi anayoiwakilisha. Huko Bukoba, kwa mfano, kivugo aghalabu hupaswa kuwa na mambo yafuatayo:-

- a) Jina halisi na/au jina la sifa la mhusika
- b) Sifa za nasaba yake ya kuumeni.

- c) Sifa za nasaba yake ya kukeni;
- d) Maelezo ya matendo matukufu aliyoyafanya;
- e) Ahadi za kutenda makubwa zaidi kwa ajili ya mkubwa wake (mzazi, mtawala, umma, n.k.)
- f) Tamati - "kujikabidhi" rasmi kwa mkubwa.

Kwa asili kivugo hakiandikwi, hutungwa papo kwa papo, lakini siku hizi baadhi ya watu wameanza kuvitunga (au kutungiwa) kwa kuandika, na halafu husoma au kusomewa kivugo hicho wakati wa sherehe inayohusika (k.m. arusi). Haya ni maingizo ya kisasa ambayo bila shaka yanaashiria kubadilika, kama si kufa, kwa sanaa hii ya kale.

#### 4.2.2.3 Tondozi

Hizi ni tungo za kusifu watu, wanyama au vitu (pembezi pia ni aina ya tondozi ambayo imekusudiwa watu wa aina fulani tu).

Ghani zenye kutondoza ni nyingi sana. Kitu chochote huweza kusifiwa, kwa mfano: mti, jiwe, mlima, kijiji, nchi, ng'ombe, mbuzi, mnyama wa pori, samaki, motokaa, baiskeli, eropleni, n.k. Miongoni mwa vitu vinavyotondozwa sana ni mifugo, hasa ng'ombe, wanyama pori, kwa mfano, simba, nyati, tembo na kiboko, na miti mikubwa. Sifa hizo wakati mwingine huwa ni za kiistiara (*allegorical*) zilizokusudiwa binadamu.

Tondozi zihusuzo wanadamu moja kwa moja ndizo nyingi zaidi. Watu husifia wapenzi wao, rafiki zao, adui zao, watani wao, wake au waume wao, watoto wao, na kadhalika.

#### 4.3.2.3 Ghani - masimulizi

Hizi ni ghani zinazotambwa ili kusimulia hadithi, historia au tukio fulani, na ambazo mara nyingi huambatana na muziki wa ala. Mtambaji wa ghani hizi huitwa *yeli* au *manju*, na kwa kawaida huwa ni bingwa wa kupiga ala fulani ya muziki. Hapa Tanzania ala zinazotumika zaidi kwa shughuli hii ni zeze, marimba,

*ligombo* (Wahehe) *enanga* (Wahaya, Waha, Wakerewe),  
ngoma na njuga.

Sifa muhimu za ghani hizi ni tatu:-

- a) Ni tungo za kishairi
- b) Husimulia hadithi au tukio kwa kirefu (ni hadithi kamili)
- c) Hutungwa papo kwa papo wakati wa utongoaji.

Tanzu za ghani - masimulizi ni nyingi. Hapa Tanzania, zifuatazo ndizo zinazofahamika zaidi.

1. Rara 2. Ngano 3. Sifo 4. Tendi

#### 4.2.3.1 Rara (ballad)

Rara ni hadithi fupi, nyepesi, ya kishairi, yenye visa vya kuisimua. Rara nyingi huimbwa, lakini pia huweza kughanwa ikiambatana na ala ya muziki. Rara nyingi husimulia mambo ya kubuni, japo zipo chache zenye kusimulia matukio ya kweli, kwa mfano kutangazwa kwa Uhuru, kesi za mauaji na kadhalika. Redio Tanzania ina kanda nyingi za rara za makabila mbalimbali ya Tanzania. Rara mara nyingi huimbwa pamoja na chombo cha muziki, k.m. zeze, marimba na *enanga*.

#### 4.2.3.2 Ngano

Tumekwisha kujadili utanzu wa ngano katika sehemu ya 2.1.1. Hapa tunautaja tu kwa vile unaingia pia katika kundi la ghani - masimulizi pindi unapoghanwa pamoja na ala ya muziki badala ya kusimuliwa tu. Sifa zake nyinginezo hubaki vilevile kama zilivyoielezwa hapo nyuma.

#### 4.2.3.3. Sifo

Sifo, kama ngano, huweza kuingia katika kundi hili wakati zinapoingiza masimulizi (*narrative*) katika utondozi wake. Baadhi ya vivugo au pembezi, badala ya

kumsifu tu mhusika, husimulia kwa kirefu matukio yanayoambatana na sifa zake, k.m. namna alivyokwenda vitani, masaibu yaliyomkuta, mapambano aliyoyashiriki au kuyashuhudia, ushindi alioupata, na namna alivyorejea. Mambo haya yaingiapo katika sifo huifanya iwe ghani - masimulizi.

#### 4.2.3.4 Tendi

Tendi ndio utanzu mashuhuri zaidi katika kundi hili la ghani - masimulizi. Utendi ni ushairi wa matendo. Ni utungo mrefu wenye kusimulia matukio ya kishujaa yenye uzito wa kijamii au kitaifa. Matukio haya huweza kuwa ya kihistoria, lakini tendi nyingi huchanganya historia na visakale au visasili.

Tangu Ruth Finnegan alipodai (1970) kuwa utanzu huu hautokei sana katika Afrika, pamekuwa na mjadala mrefu kuhusu fani hii. Wataalamu kama Okpewho (1979), Johnson (1986), Mulokozi (1987) na wengine wamethibitisha kuwa utendi ni fani iliyoenea sana katika Afrika, na wamejaribu kuonyesha baadhi ya sifa zake.

Hapa Tanzania tunao ushahidi wenye kuonyesha kuwa tendi ziko au zilikuweco katika jamii zifuatazo: Wachagga, Wahehe, Wanyambo, Waswahili, Wahaya na Wazinza. Hata hivyo, uchunguzi haujakamilika, na huenda zipo jamii nyingine zenye utanzu huu.

Utendi una sifa zifuatazo:

1. Ni masimulizi
2. Hutolewa kishairi
3. Huhusu matukio muhimu ya kihistoria au kijamii;
4. Huelezea habari za ushujaa na mashujaa.
5. Huwasilishwa kwa kughanwa (au kuimbwa) pamoja na ala ya muziki.
6. Hutungwa papo kwa papo (hautungwi kabla na kuhifadhiwa kichwani kwanza ili baadaye utolewe kwa ghibu).

7. Hivyo, hutawaliwa na muktadha wa utungaji na uwasilishaji wake kwa jamii.

Baadhi ya tendi muhimu za Kiafrika ni *Sundiata* (au *Sunjata*) (Mali, Gambia, n.k.), *Mwindo* (Zaire), *Liyongo Fumo* (Kenya, Tanzania), *Mukwavinyika* (Tanzania), *Mugasha* (Tanzania, Uganda), *Mvet* (Gabon).

Tendi ni sanaa inayoambatana na hali fulani ya kijamii, hasa ile hali yenye vuguvugu la mapambano, na yenye asasi (kama vile ufalme) zinazoweza kuidhamini sanaa ya utendi. Hivyo hii ni sanaa inayokufa, kwa vile mazingira yenye kuilea na kuirutubisha hayapo tena. Ni muhimu, basi, kuzirekodi na kuzihifadhi zile tendi chache tulizo nazo kabla hazijatoweka kabisa.

## 5. SEMI

Semi ni tungo au kauli fupi fupi za kisanaa zenye kubeba maana au mafunzo muhimu ya kijamii. Kundi hili linazo tanzu zifuatazo:

1. Methali
2. Vitendawili
3. Misimu
4. Mafumbo
5. Lakabu

### 5.1 Methali

Methali ni semi fupi fupi zenye kueleza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yaliyotokana na uzoefu wa kijamii. Mara nyingi mawazo hayo huelezwa kwa kutumia tamathali, hasa sitiari, na mafumbo. Methali ni utanzu tegemezi ambao kutokea kwake kutegemea fani zingine, kwa mfano maongezi au majadiliano mazito, katika miktadha maalumu ya kijamii. Baadhi ya methali huwa ni vielelezo au vifupisho vya hadithi fulani inayofahamika vizuri kwa wanajamii.

Methali nyingi huwa na muundo wenye sehemu mbili - sehemu ya kwanza ambayo huanzisha wazo fulani, na

sehemu ya pili ambayo hulikanusha au kulikamilisha wazo hilo. k.m. Haraka haraka/haina baraka; Tamaa mbele/mauti nyuma.

## 5.2 Vitendawili

Kitendawili ni usemi uliofumbwa ambao hutolewa kwa hadhira ili iufumbue. Fumbo hilo kwa kawaida huwa linafahamika katika jamii hiyo, na mara nyingi lina mafunzo muhimu kwa washiriki, mbali na kuwachemsha bongo zao. Vitendawili ni sanaa inayotegemea uwezo wa mtu kutambua, kuhusisha na kulinganisha vitu vya aina mbalimbali vilivyomo katika maumbile. Ni sanaa inayotendwa, inayojisimamia yenyewe, hivyo ni tofauti na methali, ambazo ni sanaa tegemezi au elelezi (*illustrative*)

## 5.3 Misimu

Misimu ni semi za muda na mahali maalum ambazo huzuka na kutoweka kutegemea mazingira maalum. Msimu ukipata mashiko ya kutosha katika jamii huweza hatimaye kuingia katika kundi la methali za jamii hiyo. Mfano:

- a) Tamutamu mahonda ukinila utakonda (Matteru, 1987:8)
- b) C.C.M - Chukua Chako Mapema

## 5.4 Mafumbo

Mafumbo ni semi za maonyo au mawaidha ambazo maana zake za ndani zimefichika. Fumbo hubuniwa na msemaji kwa shabaha na hadhira maalum, hivyo ni tofauti na methali au vitendawili ambavyo ni semi za kimapokeo.

## 5.5. Lakabu

Lakabu ni majina ya kupanga ambayo baadhi ya watu hupewa au hujipatia kutokana na sifa zao za kimwili, kinasaba, kitabia au kimatendo. Majina haya huwa ni maneno au mafungu ya maneno yenye maana iliyofumbwa. Mara nyingi majina haya huwa ni sitiari. Baadhi ya

majina humsifia mhusika, lakini mengine humkosoa au hata kumdhaliisha. Mifano mizuri ni lakabu zinazotumika katika vivugo na tendi.

Mifano:

1. Mukwavinyika (Kihehe): - Mtekaji wa Nyika (Mkwawa)
2. Ka-Itaba-Mbibi (Kihaya): - Mtoto-wa-mchanganyamipaka  
(Kaitaba : 1850 - 1888)
3. Sakarani: - Mlevi (Tom von Prince)
4. Nyundo : - Von Zelewski
5. Baba wa Taifa: Nyerere
6. Mkuki Uwakao: - Jomo Kenyatta
7. Simba wa Yuda: - Haile Selassie
8. Nyungu ya Mawe: - Nyungu (Mtemi wa Ukimbu, Unyamwezi)
9. Rwat'Enjoki (Kihaya): Mfurusha-Nyuki (Mutatembwa, Kiziba, 1865-1903)
10. Nzwala Mino-ga-Vanhu: - Mvaa meno ya watu (Kazumba, Unyanyembe)
11. Mti-Mkavu: Jenerali Mayunga

#### 6. Ngomezi (Fasihi ya ngoma)

Baadhi ya makabila huweza kupeleka habari kwa njia ya ngoma. Midundo fulani ya ngoma huwakilisha kauli fulani katika lugha ya kabila hilo. Mara nyingi kauli hizo ni za kishairi au kimafumbo.

Fasihi ya ngoma inapatikana katika makabila fulani huko Zaire, Kameruni, Nigeria, na labda hata hapa Tanzania. Utanzu huu haujachunguzwa kiasi cha kutosha, na huenda ugunduzi huu wa Kiafrika ukapotea bila kuacha kumbukumbu za kuridhisha kama hatukuufanyia kazi.

#### 7. TAMATI

Makala haya yamejaribu kuainisha na kueleza kwa



ufupi tanzu muhimu za fasihi simulizi ya Afrika. Bila shaka zipo tanzu nyingine ambazo hazikugusiwa, bali tuna imani kuwa mwalimu mwenyewe akishirikiana na wanafunzi wake, ataweza kuziba mapengo yaliyoachwa. Jambo muhimu la kuzingatia kila wakati ni kwamba fasihi simulizi hubadilika badilika kifani, kimaudhui na kiumbo kutegemea mahitaji ya muktadha wa uwasilishaji wake. Hivyo mwingiliano kati ya tanzu hizi tulizoziorodhesha ni mkubwa.

Kwa muhtasari fani za fasihi simulizi huweza kuainishwa kama inavyoonyeshwa katika jedwali A.

#### JEDWALI A

FASIHI SIMULIZI: TANZU NA FANI ZAKE

KUNDI	AINA	UTANZU	FANI
A. Mazungumzo		<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Hotuba</li> <li>2. Malumbano ya watani</li> <li>3. Ulumbi</li> <li>4. Soga</li> <li>5. Mawaidha</li> </ol>	
B. Masimulizi	Hadithi	1. Ngano	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Istiara</li> <li>2. Mbazi</li> <li>3. Kisa</li> </ol>
	Salua	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Kisakale</li> <li>2. Mapisi</li> <li>3. Tarihi</li> <li>4. Kumbukumbu</li> </ol>	
		Kisasili	
C. Maigizo		Tanzu mbalimbali kutegemea shabaha na miktadha, k.m.	

		ya watoto, ya jando, ya matanga, n.k.	
D. Ushairi	1. Nyimbo	1. Tumbuizo 2. Bembea 3. Za dini 4. Wawe 5. Tenzi 6. Tendi 7. Mbolezi 8. Kimai 9. Nyiso 10. Za vita 11. Za taifa 12. Za watoto 13. Za kazi	
	2. Maghani (a) ya kawaida	shairi juu ya mambo ya kawaida ya kijamii	
	(b) ya sifo	1. Kivugo 2. Tondozi	1. Pembezi 2. Wasifu wamambo mbali- mbali
	3. Ghani masimu- lizi	1. Rara 2. Ngano 3. Sifo 4. Tendi	
E. Semi		1. Methali 2. Vitendawili 3. Misimu 4. Mafumbo 5. Lakabu	

F. Ngomezi		1. za taarifa 2. za tahadhari 3. za uhusiano (k.m. mapenzi)	
------------	--	--	--

### TANBIHI

1. *Fasihi simulizi* ni istilahi inayotumiwa kuelezea dhana ya fasihi itolewayo kwa mdomo bila kuandikwa. Istilahi hii ina dosari, kwani neno "simulizi" halina maana ya "kitu kinachonenwa" (*oral*) bali lina maana ya "kitu kinachosimuliwa" (*narrative*). Hivyo tafsiri sahihi ya "fasihi simulizi" katika Kiingereza ni "narrative literature," siyo "oral literature." Hata hivyo, kwa kuwa istilahi hiyo imekwisha kuenea, ni vigumu kuibadilisha; hivyo inabidi tuikubali na kuitumia.

2. Kwa mfano, tazama kivugo kifuatacho:

Ni mimi Mtanzania  
 Naingia kama Seti Benjamini  
 Aliyetembea kwa miguu  
 Toka Arusha hadi Dar es Salaam  
 Tena alikufa kishujaa;

Naingia mwanamume shujaa  
 Kama Nyerere Kiongozi wa Tanzania  
 Nilikaa mtini Nikalenga kwenye chupa  
 Ni mimi aliyepiga ziwa kofi  
 Likatapika dagaa.

Naingia mtoto wa Kakwezi na Kasenene  
 Mzaliwa wa kijiji cha Tanzania  
 Masurufu ya msafiri hayaozi  
 Nasema nani mpenda kutawaliwa?  
 Je, asiyependa Ujamaa ni nani!

Kivugo hiki kilitambwa na wanafunzi wa Shule ya Msingi Kanyigo, Bukoba mwaka 1976 na kukusanywa na Ndugu Y.I. Rubanza. Kimenakiliwa katika makala ya Balisidya (Matteru) katika *Lugha Yetu* 35-36: 49 (1979-80).

#### MAREJEO

- |                                 |         |   |
|---------------------------------|---------|---|
| Balisidya, M.L.<br>(Bi Matteru) | 1979-80 | "Utafiti, Mbinu na Ukusanyaji wa Fasihi Simulizi na Hatima Yake." <i>Lugha Yetu</i> Na. 34-36, BAKITA, DSM. |
| -----                           | 1981    | <i>Kitangulizi cha Fasihi Simulizi</i> (Muswada)  |
| Biebuyck, D. na Mateena, K.     | 1969    | The Mwindo Epic of the Banyanga. University of California Press, Berkeley.                                  |
| Carrington, J.                  | 1949    | <i>Talking Drums of Africa</i> . London.  |
| Cope, T. (Mh)                   | 1968    | <i>Izibongo: Zulu Praise Poems</i> . Clarendon Press Oxford   |
| -----                           | 1977    | Oral Poetry. Cambridge University Press, Cambridge.   |
| Gabakama, Z.N.                  | 1980    | "Majigambo ya Wazanaki." Kazi Maalum, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.                     |
| Hussein, E.                     | 1975    | "On the Development of Drama in East Africa." Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Humboldt.                    |

- Ishemoi, J. 1978 "Heroic Recitations of the Bahaya of Bukoba." Project Paper, Dept. of Literature, Univ. of DSM.
- Johnson, J.W. M. 1986 *The Epic of Son-Jara*. I.U. Press, Bloomington.
- Kalugila, L. na Lodhi, A.Y. 1980 *More Swahili Proverbs from East Africa* Scandinavian Inst. of African Studies, Uppsala.
- Kamera, W.D 1978 *Hadithi za Wairaqw wa Tanzania* EALB, Arusha.
- Kamera, W.D. na Mwakasaka, C.S. 1981 *The Compliment East African Folktales Eastern Africa* Publications, Arusha.
- Kanena, G. 1975 "Heroic Recitations of the Haya: A Form of Theatre." Project Paper, Dept of Theatre Arts, Univ. of DSM.
- Kirumbi, P. 1977 *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Shungwaya, Nairobi.
- Kitemanio, A. 1977 "Mabadiliko ya Majigambo ya Kabila la Wakurya. Zamani na Wakati wa Ukoloni." Kazi Maalumu, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha DSM.
- Knappert, J. 1979 *Four Centuries of Swahili Verse*. Heinemann, London.
- Kokwijuka, M. 1983 *Traditional Wedding Songs in Buhaya: A Case Study of the Baziba*. Project Paper, Lit. Dept.

- Kunene, D.P. 1971 *Heroic Poetry of the Basotho.*  
Oxford, Clarendon.
- Makwara, V. 1980 "Utafiti wa Majigambo ya  
Wakurya." Kazi Maalum,  
Idara ya Kiswahili, Chuo  
Kikuu cha DSM.
- Malcolm X  
(Mh. A. Haley) 1963 *The Autobiography of  
Malcolm X.* Penguins,  
Harmondsworth.
- Mbele, J.L. 1983 "The Hero in the African Epic."  
A paper presented at the 26th  
Annual Meeting of the ASA,  
Boston.
- 1986 "The Liyongo Fumo Epic and the  
Scholars." (makala)
- Mbotela, J. 1934 *Uhuru wa Watumwa.* London.
- Mlacha, S. 1985 "Dhima ya Methali katika  
Malezi." *Kiswahili.* Jz. 52/1-2,  
175-186.
- Morris, H.F. 1964 *The Heroic Recitations of the  
Bahima of Ankole.* Clarendon  
Press, Oxford.
- Msuya, S.K. 1979 *Yatokanayo na Fasihi Simulizi.*  
TPH, DSM.
- Muhando, P na  
Balisidya, M. 1976 *Fasihi na Sanaa za Maonyesho.*  
TPH, DSM.
- Mulokozi, M.M. 1980 "Research on the Nanga Epic of  
the Bahaya Final Report."  
TUKI, Chuo Kikuu, DSM.-
- 1983 "Enanga : Tenzi Simulizi."

Makala, TUKI.

- 1983a "The Nanga Bards of Tanzania;  
Are They Epic Artists?  
*Research in African Literatures*  
14/3: 283-311.
- 1987 "The Nanga Epos of the Bahaya:  
A Case Study in African Epic  
Characteristics." Ph.D Thesis,  
Univ. of DSM.
- Nestor, H.B. 1978 *500 Haya Proverbs*. EALB,  
Arusha.
- Njovu, V. 1976 *Dreva wa Kwanza Tanganyika*  
1923. TPH, DSM.
- Oinas, F.J. (Ed) 1978 *Heroic Epic and Saga*. I.U.  
Press, Bloomington.
- Okot p' Bitek 1974 *Horn of my Love* Heinemann,  
London.
- Okpewho, I. 1979 *The Epic in Africa*. Columbia U.  
Press, N. York.
- Omari, C.K. na  
Mvungi, M. 1981 *Urithi wa Utamaduni Wetu*. TPH,  
DSM.
- Ong, W. 1982 *Orality and Literacy*. Methuen,  
London.
- Propp, V. 1968 *Morphology of the Folktale*.  
Univ of Texas Press, Austin.
- Raglan, Lord 1956 *The Hero*. New American Library,  
New York.
- Seitel, P. 1980 *See So That We May See*.  
*Performance and Interpretation*

*of Traditional Tales from  
Tanzania. I.U. Press,  
Bloomington.*

- Taasisi ya Mitaala  
(Elimu) 1976 *Fasihi Simulizi katika  
Sekondari*
- TAKILUKI 1983 *Fasihi Simulizi Zanzibar.  
Zanzibar*
- TUKI 1976 *Fasihi Simulizi ya Mtanzania:  
Vitendawili I Chuo Kikuu.*
- TUKI 1977 *Fasihi Simulizi ya Mtanzania:  
Hadithi I. Chuo Kikuu DSM*
- 1982 *Fasihi Simulizi ya Mtanzania:  
I-II. Chuo Kikuu*
- 1983 *Makala ya Semina ya Kimataifa  
ya Waandishi wa Kiswahili  
II: Fasihi. Chuo Kikuu DSM.*